

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

Barua zote ziadikwe na kutumwa kwa:

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Simu: +255 659 566703 (Direct line)

S.L.P. 70, SIKONGE
TABORA

Barua Pepe: ded@sikongedc.go.tz

TAREHE: 12/04/2022

**TANGAZO
LA
ZABUNI YA KUFANYA TATHIMINI YA ATHARI
ZA KIMAZINGIRA / KIJAMII KATIKA KIWANDA
CHA KUCHAKATA MAZAO YA NYUKI KATIKA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE**

LGA/121/2021/2022/NC/06

MARUDIO

1. Halmashauri ya Wilaya ya Sikunge inapenda kuwatangazia wananchi wote ikiwemo watu Binafsi na Makampuni yatakayoweza kufanya Tathimini ya Athari za Mazingira / Kijamii katika Kiwanda cha kuchakata Mazao ya Nyuki cha Halmashauri ya Wilaya ya Sikunge ambapo gharama za Kiwanda ni Tsh. 757,585,290/=


MASHARTI KWA MWOMBAJI

01. Muda wa Tathimini usizidi miezi 2 (miwili) tu
02. Kitabu cha Tathimini pamoja na Cheti viwasilishwe kwa MKurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikunge ndani ya muda wa kikanuni wa uwasilishaji wa Kitabu na Cheti.

03. Kampuni au Mwombaji aoneshe utambulisho kwamba analipa Kodi (TIN Number) na kivuli chake kiambatarishwe kwenye maombi yake
04. Kampuni iambatanishe Namba halisi ya hati ya mamlaka (POWER OF ATTORNEY) original
05. Mwombaji aonyeshe uzoefu katika kazi husika na aambatanishe vivuli vya barua ya kupata kazi toka kwa mwajiri wake alikofanyia kazi au aambatanishe kivuli cha 'Cheti cha kumaliza kazi' (Certificate of Completion)
06. Mwombaji awe amesajiliwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira
07. Mwaombaji anatakiwa kulipia Kitabu cha Zabuni kwa kazi aliyoomba kiasi cha Tsh. 15,000/= baada ya kupewa Bill / Control number / Account number toka Ofisi ya Mwekahazina / Uhasibu. Kitabu cha zabuni kinapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi (PMU). **Risiti original aliyolipia mwombaji iambatanishwe kwenye barua yake ya maombi.**
08. Maombi yote yapelekwe (yatumbwe) kwa ;

*Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge,
S.L.P 70,
SIKONGE.*

09. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni *siku ya Jumatano tarehe 29.04.2022 saa 6:00 Mchana*. Maombi yatafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ufunguzi utafanyika mbele ya waombaji au wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi mdogo uliopo katika jengo la Idara ya Elimu Sekondari
10. Maombi yatakayochelawa, schemu ya maombi, maombi ya kielektroniki, na maombi yasiyofunguliwa katika tukio la ufunguaji maombi, kwa hali yoyote maombi hayo hayatakubaliwa kwa tathmini.


Selemay M. Pandawe
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
SIKONGE


MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA - SIKONGE